Jarida la Wizara ya Afya

# Afya Habari

JARIDA LA MTANDAONI LA WIZARA YA AFYA | TOLEO, NO. 27, JANUARI 2025

TUNABORESHA AFYA

MTU NI AFYA • AFYA NI MTAJI



# TUNABORESHA AFYA

MTU NI AFYA, JALI AFYA YAKO




## BODI YA UHARIRI

**MWENYEKITI**
Dkt. Seif Shekalaghe
KATIBU MKUU

**MHARIRI MKUU**
Roida N. Andusamile

**WAHARIRI WASAIDIZI**
Emmanuel Malegi
Atley Kuni

**WAJUMBE**
Said Makora
Majid Abdulkarim
Hassan Kimweri
Shaban Juma
Cletus Sanga
Abdulwaheed Madenge
Aisha Swahibu
Antony Ishengoma

**WASANIFU**
Englibert Kayombo
Said Nyaoza

@wizara_Afyatz
www.moh.go.tz

# YALIYOMO

TANZANIA YAFANYA UWEKEZAJI MKUBWA KUKABILIANA NA VIFO VYA MAGONJWA YA MOYO ....Uk 2





SERIKALI MBIONI KUANZISHA KITUO MAALUMU CHA KUHUDUMIA MAGONJWA YA MLIPUKO, KAGERA.... Uk 3

USHIRIKIANO KATI YA TANZANIA, KOREA WAINUFAISHA SEKTA YA AFYA NCHINI..... Uk 4





SERIKALI, WADAU WAKABIDHI VIFAA KWA WAHUDUMU WA AFYA NGAZI YA JAMII ZAIDI YA 1,500 TOKA MIKOA MINNE NCHINI..... Uk 5

WATU ZAIDI YA ASILIMIA 97 WAPATIWA DAWA ZA KINGATIBA NCHINI ... Uk 6





SERIKALI, HOSPITALI ARUSHA LUTHERAN KUBORESHA HUDUMA ZA AFYA .... Uk 6

WATAALAM WA OPTOMETRIA ZINGATIENI MAWANDA YA MAJUKUMU YENU...... Uk 7





# TANZANIA YAFANYA UWEKEZAJI MKUBWA KUKABILIANA NA VIFO VYA MAGONJWA YA MOYO

**Na. Hassan Kimweri**
**DAR ES SALAAM**

Takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) za mwaka 2019 zinaonyesha kuwa, takriban watu milioni 17.9 hupoteza maisha kila mwaka kutokana na magonjwa ya moyo ikiwa ni sawa na asilimia 32 ya vifo vyote duniani ikiwemo Tanzania.

Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama alisema hayo Januari 24, 2025 kwenye uzinduzi wa Kliniki ya Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) iliyopo Oyster Bay Jijini Dar es Salaam.

"Kati ya vifo hivi, asilimia 85 husababishwa na mshtuko wa moyo pamoja na kiharusi, takwimu hizi zinaonyesha ukubwa wa tatizo la magonjwa haya Duniani na Tanzania ikiwemo," alisema Waziri Mhagama

Waziri Mhagama alisema kutokana na changamoto hiyo kubwa Duniani Serikali chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya uwekezaji mkubwa kwa kiwango cha kimataifa kwenye vifaa tiba pamoja na mitambo mbalimbali ikiwemo mashine za uchunguzi wa magonjwa kama MRI, CT- Scan pamoja na Ultrasound.

"Katika Taasisi hii ya JKCI, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amewezesha usimikwaji wa mashine Tatu za Cathlab carto kwa ajili ya upasuaji kwa njia ya tundu dogo ambapo upasuaji huu umepunguza kwa kiwango kikubwa muda wa mgonjwa kukaa hospitali," alisema Waziri Mhagama

Aidha, Waziri Mhagama alisema kuwa Serikali imeendelea kuhakikisha Hospitali zinakuwa na uwezo wa kutoa huduma za matibabu kwa wananchi katika namna mbalimbali ikiwemo programu ya tiba mkoba (Outreach Programe) ijulikanayo kwa jina la Dkt. Samia Suluhu Hassan Outreach programe.

"Upanuzi wa huduma za kibingwa za matibabu ya magonjwa ya moyo katika hospitali zetu za kanda Chato, Hospitali ya Benjamini Mkapa, Hospitali ya Kanda Mtwara na nyinginezo umeonyesha dhamira ya dhati na kutafsiri kwa vitendo dhana ya UTALII TIBA – (Medical Tourism) ambapo watu kutoka mataifa mengine kuja kutibiwa nchini," alisema Waziri Mhagama

Katika hatua nyingine Waziri Mhagama alisema utekelezaji wa mkakati wa Bima ya Afya kwa Wote unaendelea na unakwenda kuwa muarobaini wa changamoto nyingi za upatikanaji wa huduma za afya hapa nchini.

"Kwa pamoja tuungane katika kuwaelimisha wananchi umuhimu wa Bima ya Afya kwa wote kuwa ndio mkombozi wa huduma za matibabu kwa watanzania," alisisitiza Waziri Mhagama.

# SERIKALI MBIONI KUANZISHA KITUO MAALUMU CHA KUHUDUMIA MAGONJWA YA MLIPUKO, KAGERA

**Na Roida Andusamile**
**KAGERA**

Serikali ina mpango wa kujenga kituo maalum cha kuhudumia magonjwa ya mlipuko mkoani Kagera kitakachokuwa na vifaa vyote muhimu vya maabara ambavyo vitatumika kupima sampuli za vimelea vyote hatarishi sambamba na ujenzi wa kituo cha kutolea huduma za afya ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya.

Hayo yalibainishwa Januari 29, 2025 na Naibu Waziri wa Afya. Dkt. Godwin Mollel alipofika katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kagera Mhe. Fatuma Mwassa kumshukuru kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kudhibiti ugonjwa wa Marburg ulioikumba Wilaya ya Biharamulo mkoani humo ambao kwa sasa umedhibitiwa.

Dkt. Mollel alisema hatua hiyo ya Serikali inatokana na kutambua umuhimu wa kuwepo kwa kituo hicho mkoani humo kutokana na hali halisi kuwa mkoa unapakana na nchi jirani nne hivyo kuwa rahisi kupata magonjwa ya mlipuko kutokana na mwingiliano uliopo.

Akizungumzia ujenzi wa kituo cha kutolea huduma za afya alisema fedha zimeshatengwa kwa ajili ya ujenzi huo na mkoa wa Kagera ni miongoni mwa mikoa itajayopewa kipaumbele na kwamba kipaumbele cha sasa ni kuboresha huduma za afya katika ngazi ya msingi.

"Tunahitaji kufanya maboresho mengi mipakani ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa tunakuwa na watumishi ambao ni waadilifu wakati wote, alisema Dkt. Mollel.

Aidha Dkt. Mollel alisema Serikali pia itahakikisha kuwa kamati za Ulinzi na Usalama za mkoa zinapatiwa mafunzo mbalimbali ya afya kwani wamekuwa wakitoa msaada mkubwa majanga yanapotokea.

Wakati huohuo aliiagiza Bohari Kuu ya Dawa kuhakikisha kuwa inawapatia wakuu wa mikoa na wilaya nakala ya taarifa za dawa ilizosambaza katika hospitali zilizopo katka eneo husika ili kuwa na ufuatiliaji wa karibu.

Alisema utaratibu uliopo hivi sasa dawa hupelekwa moja kwa katika hospitali husika hivyo inapotokea changamoto yoyote ya upungufu wa dawa inakuwa vigumu kwa mkuu wa mkoa au wilaya kubaini uhalali wa upungufu huo.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Kagera Mhe. Fatma Mwassa alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa hatua za haraka alizozichukua kwa kutoa fedha za kukabiliana na ugonjwa wa Marburg mkoani Kagera.





# USHIRIKIANO KATI YA TANZANIA, KOREA WAINUFAISHA SEKTA YA AFYA NCHINI

**Na Cletus Sanga**
**DODOMA**

Ushirikiano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Watu wa Korea umechangia kuimarika kwa huduma za afya nchini katika nyanja za miundombinu ya vituo vya afya, vifaa tiba na mafunzo mbalimbali kwa watoa huduma za afya.

Hayo yalielezwa, Novemba 24, 2025 na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Bw. Ismail Rumatila, katika kikao kazi cha uboreshaji wa mashirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Shirika la Maendeleo kutoka Korea – KOFIH, kilichofanyika jijini Dodoma.

Bw. Rumatila alisema katika kipindi cha miaka mitano (5), Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imenufaika na ushirikiano uliopo kati yake na Korea kupitia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Nne wa Sekta ya Afya (HSSP-IV) pamoja na Mpango Mkakati wa Tano (5).

“Napenda kutoa shukrani za dhati kwa Seri kali ya Korea na taasisi ya Korea Foundation for International Healthcare (KOFIH), kutokana na msaada wenu endelevu kwa Serikali ya Tanzania, hususan kwenye sekta ya afya. Tukio la leo ni ushuhuda wa juhudi za kuimarisha ushirikiano uliopo kati ya nchi zetu mbili,” alisema Bw. Rumatila.

Aliongeza kuwa Tanzania na Korea zimeazimia kuendelea kuboresha Maabara ya Kitaifa ya Afya ya Umma kwa ajili ya udhibiti wa magonjwa ya kuambukiza, kuimarisha usimamizi wa hospitali, pamoja na ukarabati na ujenzi wa wodi maalum za watoto wachanga wagonjwa (NICU).

Kwa upande wake, Mwakilishi Mkazi wa Shirika la KOFIH Tanzania, Bw. Gyeongbae Seo, alisema Shirika hilo litaendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika kuboresha huduma za afya kwa wananchi.

# SERIKALI, WADAU WAKABIDHI VIFAA KWA WAHUDUMU WA AFYA NGAZI YA JAMII ZAIDI YA 1,500 KWA MIKOA MINNE NCHINI.

**Na abdulwaheed Madenge**
**KAGERA**

Mganga Mkuu wa Serikali Dkt. Grace Magembe amekabidhi vifaa vifaa vyenye thamani ya TZS 522,032,431, kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii zaidi ya 1,500 kwa Mikoa ya Kagera, Tabora, Mbeya na Geita.

Vifaa hivyo vilivyonunuliwa na Taasisi ya Benjamin William Mkapa (BMF) kupitia ufadhili wa Global Fund chini ya Wizara ya Afya vilitolewa Januari 24, 2025 kwa wahudumu wa Afya waliopo kwenye mafunzo katika Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Biharamulo ambapo tukio hilo lilifanyika katika Kituo cha Afya Rukaragata.

Dkt. Magembe alisema ujio wa vifaa hivyo utachangia, kuongeza hamasa miongoni mwa wahudumu hao wa ngazi ya jamii.

“Sisi tukifanya kazi vizuri kupitia vitendea kazi hivi tunavyovipokea leo kutoka BMF, Tanzania, itakuwa salama, ni kwasababu mtakuwa mnalinda, hakuna tutakachowapa kinachoendana na kazi yenu ila chochote tutakachowapa kipokeeni kwa moyo wa shukurani,” alisema Dkt. Magembe.

Akizungumza kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu wa Benjamini Mkapa Fiundation, Bw. Erick Msunyaro alisema BMF inaunga mkono jitihada na juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan za utekelezaji mpango wa wahudumu wa Afya ngazi ya jamii.

Alisema kuwa kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo Global Fund na Irish Aid katika awamu ya kwanza jumla ya wahudumu wa afya ngazi ya jamii 1943 wanapatiwa mafunzo, ikiwa ni sehemu ya mpango wa kusomesha wahudumu wa afya ngazi ya jamii 4,747 kwa awamu tofauti.

“Sisi Benjamin William Mkapa Foundation tutaendelea kushirikiana na Serikali na wadau wa maendeleo katika kuhakikisha huduma za afya kwa jamii zinaboreshwa, hususani kwa makundi yaliyo pembezoni na yenye uhitaji mkubwa zaidi, lengo letu ni kuhakikisha kila Mtanzania anakuwa salama,” alisema Bw. Mnyasuro.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Kinga kutoka Wizara ya Afya, Dkt. Ntuli Kapologwe alisema vifaa vilivyokabidhiwa ni pamoja na fulana mbili, mwamvuli, kizibao, buti, begi la mgongoni, kipima joto, koti na koti la mvua kwa kila mmoja.



# WATU ZAIDI YA ASILIMIA 97 WAPATIWA DAWA ZA KINGATIBA NCHINI



**Na Hassan Kimweri**
**DAR ES SALAAM**

Watu wapatao l 257,358 kati ya walengwa 265,217 sawa na asilimia 97 walipatiwa dawa za kingatiba za kutokomeza ugonjwa wa matende na mabusha kutoka kwenye Halmashauri za Mtama na Mtwara Mikindani kwa mwaka 2024 ili kuendelea kudhibiti na kutokomeza magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele nchini.

Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama alisema hayo Januari 30, 2025 wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye maadhimisho ya kilele cha siku ya magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele Duniani yaliyoenda sambamba na kauli mbiu isemayo "Tuungane, Tuchukue hatua, Tutokomeze Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele."

Waziri Mhagama alisema kwa upande wa ugonjwa wa usubi, watu 5,462,851 kati ya watu 6,447,157 kutoka katika halmashauri 24 walipatiwa kingatiba ya ugonjwa huo ikiwa ni sawa na asilimia 85 kwa mwaka 2024.

"Watu 1,603,425 kati ya watu 1,967,143 kutoka halmashauri saba (7) za Ngorongoro DC, Monduli DC, Longido DC, Kiteto DC, Simanjiro DC, Mpwapwa DC na Kalambo DC, walipatiwa kingatiba za ugonjwa wa trakoma (sawa na asilimia 82), watoto wenye umri wa miaka mitano (5) hadi 14 wapatao 9,896,694 walilengwa kupatiwa huduma ya kingatiba kwa ugonjwa wa minyoo ya tumbo ambapo hadi kufikia Desemba 2024 watoto 8,676,234 sawa na asilimia 88 walimeza kingatiba," alifafanua Mhe. Mhagama.

Alisema upande wa ugonjwa wa kichocho walengwa wa kumeza kingatiba walikuwa watoto 8,145,947 kati yao Watoto 6,289,884 sawa na asilimia 77 walimeza kingatiba za ugonjwa huo ambapo walengwa hao walifikiwa katika halmashauri 171 sawa na asilimia 93 ya halmashauri zote.

Aliongeza kuwa, mwaka 2024 watu wapatao 1,084 walipatiwa huduma ya upasuaji wa mabusha na wagonjwa wapatao 2,412 sawa na asilimia 67 ya matarajio wenye tatizo la vikope walirekebishwa kope bila malipo.

"Nawapongeza watumishi wa Serikali na wadau wetu waliofanikisha mazoezi hayo kwa kazi nzuri ya kuhudumia Watanzania na kuwaepusha na maradhi, kwani miongoni mwa malengo ya Serikali yetu ni kuendelea kutumia rasilimali chache zilizopo kudhibiti magonjwa yanayowasumbua wananchi wake," alisema Mhe. Mhagama.

Shabaha ya utoaji wa kingatiba ni kutokomeza magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, hivyo Waziri Mhagama alitumia fursa hiyo kuwaasa wananchi kujitokeza pindi mazoezi hayo yanapotangazwa kwenye maeneo yao.



# SERIKALI, HOSPITALI ARUSHA LUTHERAN KUBORESHA HUDUMA ZA AFYA

**Na Shaban Juma**
**DODOMA**

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, Mhe. Elibariki Kingu, ameiagiza Wizara ya Afya kuchukua hatua za haraka kuingia makubaliano na Hospitali ya Arusha Lutheran Medical Center kwa lengo la kuzisaidia kwa ruzuku, vifaa tiba, dawa, na wahudumu wa afya.

Mhe. Kingu alitoa agizo hilo Januari 23, 2025 wakati wa kikao cha kamati kilichofanyika baada ya wasilisho la Hospitali ya Arusha Lutheran Medical Center, ambayo ilielezea mafanikio yake ya utoaji wa huduma za afya kwa miongo kadhaa, hivyo ni muhimu kushirikiana na Serikali ili kuboresha sekta ya afya.

Kamati hiyo pia ilitoa mapendekezo ya kuboresha ufanisi wa huduma hizo, ikiwemo kufunga mifumo ya kielektroniki ya afya (EHMS) kwani hospitali zinapaswa kufungwa mfumo huo ili kudhibiti ubadhirifu wa fedha na kuondoa malipo ya fedha mkononi, akitolea mfano wa mafanikio ya mfumo huo katika Hospitali ya KCMC.

Aidha Mhe. Kingu alisema Kamati imependekeza NHIF iisaidie hospitali hiyo kwa kukopesha vifaa tiba ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi sambamba na watumishi watakaopelekwa hospitalini hapo wenye uwezo mkubwa, hasa kwa kuzingatia kwamba Arusha ni mji wa utalii na huduma zinazotolewa zinapaswa kuwa za viwango vya kikanda.



# WATAALAM WA OPTOMETRIA ZINGATIENI MAWANDA YA MAJUKUMU YENU

**Na Aisha Swahibu**
**DODOMA**

Wanataaluma ya optometria nchini wametakiwa kutoa huduma kwa wananchi kwa kuzingatia mawanda ya majukumu yao pamoja na sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya taaluma zao.

Kauli hiyo ilitolewa Januari 16, 2025 na Mkurugenzi Msaidizi wa Rasilimali Watu wa Wizara ya Afya Bi. Grace Sheshua wakati wa mafunzo ya maadili na hafla ya utoaji vyeti kwa wataalam wa kada ya optometria ngazi ya shahada na stashahada waliopata usajili wa kudumu na usajili wa awali, Jijini Dodoma.

Bi. Sheshua alihimiza Mabaraza ya kitaaluma kuhakikisha wataalam hao wanaowasimamia wanatoa huduma kwa kufuata miongozo hiyo na kufatilia mienendo yao wakiwa mahala pa kazi.

"Baadhi ya wataalam wamekuwa wakitekeleza majukumu yasiyo ya kwao na kusababisha changamoto mbalimbali za uoni kwa jamii, hivyo ni vyema kufanya kazi ambayo una utaalam nayo pekee," alisema Bi. Sheshua.

Alisema Serikali kupitia Wizara ya Afya imeendelea kuweka juhudi kubwa katika huduma za macho kwa kuhakikisha kuwa inatekeleza mpango Mkakati wa Kitaifa wa Afya ya Macho wa 2022- 2027, lengo likiwa ni kupunguza upofu na ulemavu wa macho miongoni mwa Watanzania.

"Wizara ya Afya kupitia mpango wa Taifa wa Huduma ya Macho imejitahidi kuhakikisha kuwa, kila hospitali ya mkoa na hospitali nyingi za wilaya zinakuwa na idara ya macho inayotoa huduma ya kina ya macho ikiwa ni pamoja na huduma za optometria," alifafanua Bi. Sheshua.

Awali akimkaribisha Mkurugenzi Msaidizi Rasilimali Watu, Mwenyekiti wa Baraza la Optometria Tanzania Dkt. Anna Sanyiwa aliwataka wataalam hao kuipenda na kuionea fahari taaluma yao na kwenda kutoa huduma bora za macho kwa Watanzania pamoja na kujikita katika bunifu mbalimbali za fani hiyo, ili kuzidi kuikuza taaluma hiyo.

Naye Msajili wa Baraza la Optometria Bw. Sebastiano Milanzi alitoa rai kwa wataalam hao kuyazingatia yale yote waliyofundishwa wakati wa mafunzo hayo na kuonya juu ya ukiukwaji wa sheria, kanuni na miiko ya kitaaluma na kusema kuwa Baraza litachukua hatua kali ikiwa ni pamoja na kusitisha au kufuta usajili endapo ukiukwaji huo utajitokeza kwa yeyote yule.





# WAZIRI MHAGAMA ALITAKA BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA KUSIMAMIA SHERIA, MIIKO

**Na Hassan Kimweri**
**DODOMA**

Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama amelitaka Baraza jipya la Wauguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) kuwachukulia hatua kali wauguzi na wakunga watakaokiuka misingi ya sheria na miiko ya taaluma zao.

Waziri Mhagama alitoa agizo hilo Januari 15, 2025 wakati akizindua Baraza jipya la 63 la Uuguzi na Ukunga Tanzania, jijini Dodoma, wenye kauli mbiu isemayo “Wauguzi na Ukunga ni Watu Maalum kwa Kazi Maalum”.

"Baraza lenu lina kazi nyingi, miongoni mwa kazi zenu mnatakiwa kuhakikisha watumishi mnaowasimamia wanafanya kazi kwa weledi mkubwa ili kuwa na huduma zenye tija na ufanisi," alisema Waziri Mhagama.

Aidha, Waziri Mhagama alilitaka Baraza hilo kuanzisha kanzi data inayoweza kufatilia wauguzi na wakunga wote nchini ili kurahisisha ufuatiliaji wa mienendo yao na upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

“Niwaelekeze Baraza, kuwa na mifumo mizuri inayohifadhi data za wauguzi na wakunga kuanzia walipo kwa sasa na mienendo yao, pia kuwatambua wauguzi na wakunga ambao hawana ajira ili kutengeneza mazingira mazuri ya kujiajiri kwa wataalam hao," alisema Waziri Mhagama.

Awali akimkaribisha Waziri wa Afya Mkurugenzi wa Idara ya Uuguzi na Ukunga kutoka Wizara ya Afya Bi. Ziada Sella alilitaka Baraza hilo kusimamia mawasiliano pamoja na lugha za staha kwa wananchi wanaowapatia huduma pamoja na kusimamia usajili wa wauguzi na wakunga sambamba na kutoa mafunzo mahala pa kazi kwa wataalam hao.

“Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Baraza linaendela kusimamia mawasiliano na lugha nzuri kwa wataalam dhidi ya wananchi, eneo hili ni muhimu sana kwa sababu ndio matibabu yanaanzia hapo,” alisema Bi. Ziada.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Baraza la Wauguzi na Ukunga Tanzania Prof. Lilian Msele aliishukuru Wizara ya Afya kwa kuteau wajumbe wa Baraza hilo na kuahidi kutekeleza kwa vitendo maelekezo yote aliyoyatoa Waziri Mhe. Mhagama.

# M-MAMA YAOKOA MAISHA, VIFO VYAPUNGUA



**Na Shaban Juma**
**DODOMA**

Serikali imepunguza vifo vya watoto wachanga kwa kiwango kikubwa, huku mfumo wa usafiri wa dharura, M-Mama ukichangia kuokoa maisha ya akina mama na watoto wachanga nchini.

Akizungumza jijini Dodoma Januari 15, 2025 mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kwenye ukumbi mdogo wa Bunge, Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Godwin Mollel, kwa niaba ya Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama alisema kuwa vifo vya watoto walio chini ya miaka mitano vimepungua kutoka 67 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2015/16 hadi 43 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2022.

"Tanzania ni miongoni mwa nchi chache zilizofanikiwa kufikia Malengo ya Milenia kwa kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitano hadi angalau 54 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2015," alisema Dkt. Mollel.

Dkt. Mollel alieleza kuwa mfumo wa M-Mama, unaoratibu usafiri wa dharura kwa akina mama na watoto wachanga, umefanikiwa kuokoa maisha ya watu zaidi ya 5,000 tangu ulipoanzishwa, kwani zaidi ya akinamama na watoto wachanga 120,000 wamesafirishwa kwa dharura kupitia mfumo huo.

Alisema, hatua imeongeza mara mbili upatikanaji wa huduma za usafiri wa dharura katika maeneo yenye changamoto.

"Mfumo wa M-Mama umeondoa changamoto ya ukusanyaji wa data, ambapo awali taarifa za rufaa zilihifadhiwa ndani ya vitabu vya usajili kwenye vituo vya afya. Sasa taarifa hizi zinapatikana kwa urahisi kupitia mifumo yetu ya kidigitali," aliongeza Dkt. Mollel.

Aidha, mfumo huo unatarajiwa kuwa na mafanikio makubwa zaidi, huku Wizara ya Afya ikipanga kuongeza uhamasishaji wa jamii na kuboresha zaidi huduma katika maeneo yenye mahitaji makubwa.

Pia, Dkt. Mollel alisema zaidi ya watoa huduma 20,000 wanapewa mafunzo rasmi na elekezi kazini kupitia mpango wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ili kuhakikisha huduma za afya kwa mama na mtoto zinaimarishwa.

Serikali imeahidi kuendelea kushirikiana na wadau kuhakikisha huduma za afya kwa watoto wachanga na akina mama zinaboreshwa zaidi, huku lengo likiwa ni kupunguza vifo zaidi na kuimarisha ustawi wa familia nchini.



# WIZARA, MIKOA TISA WAJIPANGA KUPAMBANA NA KIFUA KIKUU

**Na Aisha Swahibu**
**DODOMA**

Waganga Wakuu wa mikoa tisa (9) na Waratibu wa Kifua Kikuu na Ukoma wa mikoa wameonesha utayari wao wa shughuli za uibuaji wa wagonjwa wa kifua kikuu kwenye mapango harakishi wa kuwaibua na kuwaweka katika matibabu wagonjwa wa Kifua Kikuu zaidi ya 14000 wakiwemo watoto.

Hayo yalibainishwa na Kaimu Mganga Mkuu wa Serikali Dkt. Ahmed Makuwani Januari 8, 2025 wakati akifungua kikao kazi cha Waganga Wakuu wa mikoa, Waratibu wa Kifua Kikuu na Ukoma wa mikoa na Wataalam wa Wizara ya Afya kujadili utekelezaji wa Mpango harakishi wa uibuaji wagonjwa wa Kifua Kikuu.

Alisema mpango huo unategemewa kutekelezwa ngazi ya vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na ngazi ya jamii hususani makundi yaliyo maeneo hatarishi ya maambukizi ya ugonjwa wa Kifua Kikuu kama vile wachimbaji wa madini, wavuvi, wadungaji sindano, wafungwa na makundi mengine katika mikoa tisa (9) na halmashauri 76 Tanzania Bara.

Dkt. Makuwani alisema Tanzania inaendelea kukabiliana na changamoto ya kuwapata wagonjwa wa Kifua Kikuu na kuwaweka kwenye matibabu ili kuiondoa nchi kwenye kundi la nchi 30 zinazochangia asilimia 87 ya wagonjwa wote wa Kifua Kikuu Duniani.

"Januari 6, 2025 Waziri wa Afya, Mhe. Jenista Mhagama alizindua rasmi mpango wa kitaifa wa kuharakisha uibuaji wa wagonjwa wa Kifua Kikuu katika mikoa tisa (9) ya Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Kagera, Mara, Simiyu, Shinyanga, Ruvuma na Tanga na kugawa mashine 185 za ugunduzi wa vimelea vya ugonjwa wa Kifua Kikuu na alitoa maelekezo yanayolenga kuongeza juhudi za uibuaji wagonjwa wa Kifua Kikuu nchini," alisema Dkt. Makuwani.

Dkt. Makuwani alisema, lengo ni kupunguza visa vya Kifua Kikuu kwa 50% na vifo kwa 75% ifikapo 2025 ikilinganishwa na takwimu za mwaka 2015, ambapo kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2023, Tanzania kupunguza visa vya Kifua Kikuu kwa asilimia 40.

# TANZANIA, JAPAN ZATIA SAINI HATI YA USHIRIKIANO MIRADI YA AFYA NCHINI

**Hassan Kimweri**
**DAR ES SALAAM**

Tanzania na Japan zimetia saini hati ya Makubaliano (MoU) ya utekelezaji miradi ya huduma za Afya lengo likiwa ni kuboresha huduma hizo na kuhuisha ushirikiano kwa kipindi cha miaka mitano (5) kwa kuzingatia vipaumbele vya pamoja.

Utiaji saini wa makubaliano hayo ulifanyika Januari 8, 2025 katika ukumbi wa Wizara ya Afya kati Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama na Balozi wa Japan aliyemaliza muda wake Mhe. Yasushi Migawa.

Akizungumza mara baada ya utiaji saini wa makubaliano hayo Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama aliyataja maeneo ya ushirikiano kuwa ni uboreshaji wa huduma nje ya vituo, rufaa na huduma za kibingwa katika ngazi zote za utoaji huduma za Afya.

Aidha Waziri Mhagama alitaja maeneo mengine ya ushirikiano kuwa ni kuboresha huduma za uzazi, afya ya mama na mtoto, kuzia na kudhibiti magonjwa ya milipuko na matukio mengine ya dharura za Afya.

Mhe Mhagama alisema Tanzania ipo mbioni kujenga kituo cha umahiri cha usambazaji wa teknoliojia ya tiba ya figo hapa nchini pamoja na nchi jirani, suala ambalo litaijengea Tanzania heshima kubwa katika anga za kimataifa.

Naye Balozi wa Japan nchini Tanzania aliyemaliza muda wake Mhe. Yasushi Migawa alisema Serikali ya Japan inaweka vipaumbele katika usalama wa binadamu ndio maana itaendelea kuwekeza katika huduma za afya kwa nchi za Afrika kama ambavyo imekuwa ikifanya katika nchi za Asia.

Aidha Balozi Migawa aliongeza kuwa Serikali yake imekuwa ikitekeleza miradi ya afya kupitia mashirika makubwa ya nchini Japan, akibainisha kuwa miradi hiyo imekuwa ikitekelezwa kupitia shirika la JICA na mashirika mengine yanayojitolea kutoa elimu ya juu ya fani ya udakitari nchini mwake.

Balozi Migawa aliyataja maeneo mengine muhimu ambayo Serikali yake imekuwa ikitekeleza kwa upande wa afya ni pamoja na kusaidia huduma za upandikizaji wa figo hospitali ya Benjamini Mkapa ikiwemo ufadhili wa masomo nchini Japan.



# WEKENI MIKAKATI YA PAMOJA KATIKA TIBA ASILI TUIDUMISHE



**Na Aisha Swahibu**
**DAR ES SALAAM**

Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Afya zimetakiwa kuweka mikakati madhubuti ya ushirikiano katika sekta ya tiba asili ili huduma zinazotolewa zinakidhi viwango vya usalama na ufanisi.

Hayo yalielezwa Januari 31, 2025 na Mkurugenzi wa Huduma za Tiba, Dkt. Hemed Nyembea wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Kujadili Mikakati ya Afya na Huduma za Tiba Asili, jijini Dar es Salaam.

" Tiba za asili imekuwa na mchango mkubwa kwenye maisha ya watu kwa karne nyingi na katika miaka ya hivi karibuni, tumepiga hatua kubwa, ikiwa ni pamoja na kuingiza huduma za tiba asili zipatazo saba katika hospitali saba za rufaa nchini," alisema Dkt. Nyembea.

Dkt. Nyembea alisema ushirikiano huo unapaswa kuhusisha taasisi za utafiti, vyuo vya elimu ya juu, na wadau wa tiba asili ili kuwezesha tafiti za kina, usajili wa dawa, na uboreshaji wa mifumo ya udhibiti.

Alitumia fursa hiyo pia kuwashukuru wadau wote, hususan taasisi za utafiti na elimu ya juu kwa mchango wao wa hali na mali katika kuhakikisha sekta ya tiba za asili inakua na kustawi.

Ushirikiano wenu ni muhimu katika kufanikisha malengo yetu ya muda mrefu," Aliongeza Dkt. Nyembea

Aidha, Dkt. Nyembea aliitaka Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) kufanya tafiti za kina kwa wataalam wa tiba asili ya Mwafrika kwani NIMR inapaswa kufanya tafiti za kina kuhusu vyanzo vya dawa zinazotumika na kuhakikisha kuwa zinatunzwa vizuri na kuendelea kuzalishwa kwa wingi kwenye huduma zao.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala, Prof. Joseph Otieno, ameeleza kuwa dawa zinazotengenezwa na wataalamu wa tiba asili zimepiga hatua kubwa katika ubora, usalama na ufanisi.

Ushirikiano wetu utaendelea kuwa chachu ya mafanikio katika kukuza tiba asili kwa manufaa ya taifa letu kwa kizazi cha sasa na kijacho.

# UGONJWA WA MALARIA NA JITIHADA ZA KUUTOKOMEZA NCHINI



**Na atley Kuni**

Malaria ni mojawapo ya changamoto kubwa za afya inayokumba nchi nyingi barani Afrika, ikiwemo Tanzania, ambapo kwa upande wa Tanzania bara kiwango cha maambukizi ya malaria kulingana na takwimu za mwaka 2022 ni asilimia 8.1. Hata hivyo, Tanzania imeweka malengo makubwa ya kutokomeza malaria ifikapo mwaka 2030. Kupitia jitihada mbalimbali za kitaifa na kimataifa, nchi imeonyesha maendeleo makubwa katika kupambana na ugonjwa huu.

Kwa mjibu wa takwimu hizo za utafiti wa viashiria vya malaria katika jamii wa mwaka 2022, kiwango cha maambukizi ya ugonjwa wa malaria vimepungua kwa asilimia 45 kutoka asilimia 14.8 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 8.1 mwaka 2022.

Mikoa mitano inayoongoza kwa maambukizi ya ugonjwa wa malaria nchini ni Tabora (23.4%), Mtwara (19.7%), Kagera (17.5%) Shinyanga (15.6%) na Mara (15.1%) Hata hivyo idadi ya mikoa yenye kiwango cha juu cha maambukizi ya ugonjwa wa malaria imepungua kutoka mikoa 14 mwaka 2015 hadi kufikia mikoa 8 mwaka 2023. Mikoa yenye kiwango cha chini kabisa cha maambukizi ya malaria (chini ya asilimia moja) imeongezeka kutoka mikoa 6 mwaka 2017 hadi kufikia mikoa 9 mwaka 2022. Mikoa hiyo ni Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Dodoma, Songwe, Mwanza, Dar es Salaam, Iringa na Singida.

Miongoni mwa ya njia bora ya kujikinga na malaria ni matumizi ya vyandarua vyenye viuatilifu. Serikali, kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo kama vile Global Fund na Mfuko wa Rais wa Marekani katika mapambano dhidi ya malaria (PMI), inasambaza mamilioni ya vyandarua vyenye viuatilifu hapa nchini kupitia njia mbalimbali ikiwemo kaya,kliniki kwa wajawazito na watoto chini ya mwaka mmoja na shule za msingi. Kampeni kama “Ziro Malaria inaanza na Mimi” zimeongeza uelewa kuhusu umuhimu wa vyandarua vyenye viuatilifu, hatua ambayo imesaidia kupunguza maambukizi ya malaria kwa kiasi kikubwa.

Pamoja na jitihada hizi za matumizi ya vyandarua, bado wapo baadhi ya wanajamii ambao wamekuwa sio waaminifu hasa pale wanapobadili matumizi ya vyandarua kwa kuvulia samaki, kufunikia vifaranga vya kuku/Bata na wengine hata kudiriki kugeuza vyandarua kama furushi la kubebea chupa zilizoisha muda wake, hii haina afya kwa mapambano yaliyo mbele yetu yakutokomeza malaria ifikapo mwaka 2030 lazima watu hawa wajitathmini kwa hali kama hii.

Mbali na Vyandarua njia nyingine za kujikinga na malaria ni unyunyiziaji wa viuadudu vya Kibaiolojia kwenye mazalia ya mbu pamoja na usafi na utunzaji wa mazingira Afua hii inalenga kupunguza mbu waenezao malaria wakiwa katika hatua ya viluilui na hatimaye kupunguza maambukizi ya malaria.

Mafanikio makubwa yamepatikana katika mapambano ya malaria hapa nchini, ikiwemo Serikali kuimarisha upatikanaji wa dawa na bidhaa muhimu za malaria kwenye vituo vyote vya umma vya kutolea huduma za afya hapa nchini ambapo upatikanaji wa bidhaa hizo ni zaidi ya asilimia 90. Kwa sasa dawa mseto za Malaria, Vipimo vya haraka vya malaria (mRDTs) vinapatikana bila malipo na wagonjwa wa malaria wanapata matibabu sahihi na kwa wakati. Juhudi hizi zimepunguza vifo vinavyotokana na malaria kwa asilimia 78 kutoka vifo 6,311 kwa mwaka 2015 hadi kufikia vifo 1,392 kwa mwaka 2024 na hivyo kuongeza matumaini ya kutokomeza ugonjwa huu.

Ili kuendelea kujikinga na malaria wananchi wanahamasishwa kuondoa maji yaliyotuama ambayo ni mazalia ya mbu na kutunza mazingira kwa ujumla, aidha, elimu na hamasa kwa umma ni nguzo muhimu katika mapambano dhidi ya malaria.

Kupitia vyombo vya habari, machapisho mbalimbali, vikundi vya kijamii, matangazo ya vipaza sauti, shule na njia nyingine mbalimbali, wananchi wanapewa elimu kuhusu kuzuia na kutibu malaria, hatua hii imeongeza matumizi ya huduma za afya na kuboresha ushirikiano wa jamii na kudhibiti ugonjwa huu.

Katika hatua hii, hivi karibuni zaidi ya waandishi wa habari 25 kutoka Klabu ya waandishi wa habari mkoa wa Shinyanga walipewa elimu ili wawe mabalozi sahihi wakati wa kuandikisha, kugawa na hata kufuatilia matumizi sahihi kwa vyandarua zaidi ya milioni 2.5 vitakavyogawiwa mkoani humo kupitia kampeni ya ugawaji vyandarua kwenye kaya kwa uwiano wa chandarua kimoja kwa watu wawili.

Pamoja na hatua hii ya kuwahusisha kundi la wanahabari, ifahamike kuwa, vita hivyo lazima vipiganwe na kila mzalendo wa nchi hii na hili linathibitishwa na Taasisi za utafiti kama “Ifakara Health Institute” Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) na nyinginezo, ambazo zinaendelea na juhudi za kugundua mbinu mpya za kudhibiti malaria hapa nchini.

Mathalani tafiti kuhusu tabia za mbu na vimelea vya malaria zimekuwa ni jitihada za taasisi hizi na imekuwa msaada mkubwa, lakini pia, Tanzania kama nchi imekuwa miongoni mwa nchi zinazojaribu chanjo ya malaria, RTS, S /AS01E (Mosquirix), ambayo inaonyesha matumaini makubwa mafanikio haya yanaonesha mwanga na matumaini ifikapo 2030.

Jitihada za Tanzania zinatokana na msaada mkubwa na msukumo kutoka kwa mashirika ya kimataifa kama Shirika la Afya Duniani (WHO), Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (Global Fund) na Mpango wa Rais wa Marekani wa Kupambana na Malaria(PMI). Ushirikiano huu umewezesha upatikanaji wa rasilimali, vifaa vya kisasa, na utaalamu wa kitaalama, hatua inayochochea mafanikio zaidi kwenye mapambano dhidi ya malaria.

Kwa kuzingatia jitihada hizi, Tanzania ipo kwenye njia sahihi ya kutokomeza malaria ifikapo mwaka 2030. Hata hivyo, mafanikio haya yanahitaji juhudi za ziada, hususan kwenye kudhibiti usugu wa mbu dhidi ya viuatilifu na kuimarisha upatikanaji wa rasilimali za kutosha. Ushirikiano wa karibu kati ya Serikali, mashirika ya kimataifa, na jamii ni msingi wa kufanikisha azma hii.

Kwa ujumla, jitihada za Tanzania siyo tu kwamba zimepunguza mzigo wa malaria, bali pia zimeonyesha kuwa ugonjwa huu unaweza kudhibitiwa na hatimaye kutokomezwa. Ni jukumu la kila mmoja kushiriki katika mapambano haya kwa mustakabali bora wa afya ya jamii na maendeleo ya taifa.



*Afisa Uvuvi wilaya Simanjiro Bw. Victor Nyenga na Mtendaji wa Kijiji cha Magadini Wilson Lawi, Wakiteketeza Vyandarua vilivyo badilishiwa Matumizi na Wavuvi haramu katika Bwawa la Nyumba ya Mungu.*

# WAHUDUMU WA AFYA WAPEWA MAFUNZO KUKABILIANA NA MAGONJWA YA YALIYOKUA HAYAPEWI KIPAUMBELE

**Na Aisha Swahibu**
**MTWARA**

Serikali kupitia Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Shirika la Kongwa Trachoma Project (KTP) imeendelea kupambana na magonjwa yaliyokua hayapewi kipaumbele kwa kuwapatia mafunzo wahudumu wa afya kuanzia ngazi ya msingi ili kuongeza uelewa wa namna bora ya kushughulikia magonjwa hayo.

Hayo yalibainishwa Januari 31, 2025 na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Nanyamba, Bw. Abdallah Kapende wakati wa maadhimisho ya Magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele mkoani Mtwara.

"Tuhamasishe umma kufahamu namna magonjwa haya yanavyoambukizwa, dalili zake na jinsi ya kuyatibu, hususan kwa wale waliokwisha athirika," alisema Bw. Abdallah.

Bw. Abdallah alisema Kambi hii imefanyika wilaya ya Nanyamba ikiwa ni sehemu ya kampeni inayolenga kutoa huduma katika wilaya sita(6) za mkoa wa Mtwara.

Alisema Kampeni hiyo inalenga kuwafikia wananchi wengi zaidi kwa kuwapatia elimu, uchunguzi, na matibabu ya magonjwa haya ili kupunguza maambukizi.

Kwa upande Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Dkt. Benedicto Ngaiza aliishukuru Serikali kwa kuendelea kuleta miradi inayogusa sekta ya afya na aliahidi kuwa watausimamia mradi huu kwa ukaribu ili kuhakikisha unatoa huduma bora kwa wananchi.

Naye, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kinga Wizara ya Afya, Dkt. Otilia Gowelle, alisema Mkoa wa Mtwara umekuwa kinara katika utambuzi wa magonjwa yasiyopewa kipaumbele.

Alisema hilo limefanikiwa kwa kushirikisha wahudumu wa afya ngazi ya jamii ambao hutembelea kila nyumba na kila kata kuwatambua wagonjwa mapema na kuwapeleka kwenye vituo vya afya kwa matibabu.

Dkt. Otilio alisisitiza kuwa magonjwa kama kichocho na minyoo yanayoathiri watoto yanahitaji juhudi za pamoja kuyadhibiti.

Dkt. Gowelle alisema Serikali imeweka mikakati ya kumezeshwa dawa kila mwaka kwa watoto ili kupunguza maambukizi.



# WAZIRI MHAGAMA ATEKELEZA MAAGIZO YA MAKAMU WA RAIS UJENZI WA CHUO CHA WAUGUZI

**Na Hassan Kimweri**
**KILIMANJARO**

Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama ametekeleza kwa vitendo maagizo ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Isdor Mpango ya ujenzi wa chuo cha wauguzi kitakachojengwa pembeni ya hospitali ya wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro.

Waziri Mhagama alisema hayo Januari 7, 2024 akiwa katika ziara ya siku mbili mkoani Kilimanjaro kwa lengo la kukagua na kuzindua miradi ya sekta mbalimbali ikiwemo ya sekta ya afya katika Wilaya ya Rombo pamoja na wilaya ya Same ambako alizindua wodi ya wazazi iliyopo katika kituo cha afya Mkuu - Rombo.

"Ndugu zangu Serikali ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan haijawahi kupoa, hasa kwenye sekta ya afya, tupo macho kupokea maelekezo na kuyatekeleza, sasa ujenzi wa chuo chetu cha wauguzi utaanza mwezi wa tatu, ili kupunguza tatizo la watumishi ndani ya wilaya, mkoani na Tanzania kwa ujumla," alisema Waziri Mhagama.

Waziri Mhagama alisema tayari Wizara ya Afya imetenga Shilingi Bilioni Moja ili kuanza haraka iwezekanavyo ujenzi huo ambao utakuwa na uwezo wa kuchukua vijana zaidi ya 600 na vijana wa bweni wasiopungua 400.

Aidha, Waziri Mhagama alisema ndani ya miaka mitatu ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali yake imetoa Shilingi Bilioni 82 katika wilaya ya Rombo ili kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo miradi katika sekta ya afya ya ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya, zahanati pamoja na hospitali.

"Tunaposema Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni wa viwango vya juu tunamaanisha kwa sababu miaka iliyopita Rombo haijawahi kupokea fedha nyingi kiasi hiki na hizo Bilioni 82 ni kati ya Bilioni 956 zilizoletwa katika mkoa huu wa Kilimanjaro, hivyo tuna kila sababu ya kumshukuru Rais kwa kuamua kuibeba Tanzania ukiwemo mkoa wa Kilimanjaro kwa kiwango tofauti," alisema Waziri Mhagama.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe. Nurdin Babu alimshukuru Rais Dkt. Samia kwa mapenzi makubwa ya wananchi wake wa mkoa huo, ambapo katika kipindi cha miaka mitatu mkoa huo umepokea Shilingi Bilioni 956 za maendeleo.





# TANZANIA YAPOKEA MSAADA WA VIFAA TIBA VYA SHILINGI MILIONI 125 KUTOKA CHINA

**Na Hassan Kimweri**
**DAR ES SALAAM**

Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China imetoa msaada wa vifaa tiba vyenye thamani ya Shilingi Milioni 125 vilivyokabidhiwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili Jijini Dar es Salaam ambao ni sehemu ya utekelezaji wa makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na China.

Wakati akipokea vifaa hivyo Januari 24, 2025 Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama alisema kuwa msaada huo ni ushahidi mkubwa wa mshikamano imara na utayari wa pamoja katika kuimarisha huduma za afya nchini ili wananchi wapate huduma bora za afya.

"Msaada huu ni mchango muhimu sana katika kukabiliana na mahitaji ya huduma za afya kwa wananchi, pia katika kuimarisha ushirikiano na urafiki kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, hivyo tuendelee kudumisha umoja wetu ulioanzishwa na viongozi wetu hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Mwenyekiti Mao Zedong," alisema Waziri Mhagama

Waziri Mhagama aliutaka uongozi wa Hospitali ya Muhimbili kuvitunza vifaa hivyo, endapo vitaharibika wavitengeneze haraka ili viendelee kutumika ipasavyo katika kuimarisha utoaji wa huduma na kuleta matokeo chanya katika hospitali hii na wananchi waendelee kupata huduma bora za afya.

Aidha, Waziri Mhagama alisema Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China imeendelea kutuma timu ya wataalam wa afya nchini kila baada ya miaka miwili ambayo timu hiyo imekuwa msaada mkubwa sana katika hospitali kwa kutoa mafunzo kwa ngazi ya ubingwa na ubingwa bobezi kwa wataalam wa ndani.

Kwa upande wake Balozi wa Jamhuri ya watu wa China nchini Tanzania Mhe. Chen Ming Jian alisema kuwa China itaendelea kushirikiana na Tanzania katika kuboresha huduma za afya kwa wananchi wake, ikiwemo kutoa vifaa tiba ambapo hadi sasa wameweza kudumisha ushirikiano huo kwa zaidi ya miaka 60.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili Prof. Mohamed Janabi aliishukuru Wizara ya Afya kwa kudumisha ushirikiano na watu wa china.

"Leo tunapopokea vifaa hivi vyenye thamani ya Shilingi Milioni 125 ni dhahiri kwamba ushirikiano huu unamanufaa makubwa sana Tanzania hasa katika Sekta ya Afya,"alisema Dkt. Janabi.

# UTAFITI WAFICHUA UKWELI MATUMIZI VIDONGE VYA DHARURA VYA UZAZI

**Na Cletus Sanga**
**DAR ES SALAAM**

Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) imebainisha kuwa utafiti wa matumizi ya vidonge vya dharura vya uzazi wa mpango (P2) ni ya kiwango cha chini ikilinganishwa na taswira inayotolewa na baadhi ya vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

Akizungumzia utafiti huo Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto Dkt. Nassoro Mzee Januari 23, 2025 jijini Dar es Salaam alisema elimu kuhusu matumizi ya P2 ni muhimu kutolewa katika jamii ili kuondokana na taarifa potofu zinazozunguka kuhusu dawa hizo.

Dkt. Nassoro alisema kuwa matumizi ya vidonge vya P2 ni kwa ajili ya dharura pekee na siyo njia ya kawaida ya uzazi wa mpango.

Aliongeza kuwa utafiti huo umeonyesha kuwa mwaka 2023, ni wanawake wawili tu kati ya 10,000 waliotumia P2 siku yoyote.

Katika ngazi ya wilaya, ni wanawake saba (7) tu kati ya milioni moja walioripotiwa kutumia vidonge hivyo. Kwa wanawake wenye umri wa miaka 20-44, ni watatu tu kati ya elfu 10 waliotumia P2 kwa mwaka mzima.

"P2 ni kwa dharura pekee na si njia ya kawaida ya uzazi wa mpango," alisisitiza Dkt. Mzee.

Aliongeza kuwa uzazi wa mpango ni kipaumbele cha Wizara ya Afya kwa sababu unachangia kupunguza vifo vya mama na mtoto, huku ukiwawezesha wanawake kupanga familia zao kwa uhuru.

Alisema, Serikali itaendelea kushirikiana na wadau wa afya ili kuboresha upatikanaji wa huduma bora za uzazi wa mpango kote nchini.

Dkt. Mzee alitoa wito kwa Kitengo cha Mawasiliano cha Wizara ya Afya kuhakikisha matokeo ya utafiti huo yanawafikia wananchi, ili kuimarisha uelewa wa matumizi sahihi ya P2 na njia nyingine za uzazi wa mpango.

Utafiti huo, ulioshirikisha maeneo ya Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Mbeya, Mtwara, na Mwanza, pia uliangazia imani na mitazamo ya jamii kuhusu matumizi ya P2.

Serikali imejipanga kuhakikisha huduma bora za uzazi wa mpango zinapatikana kwa wanawake na wasichana kote nchini kwa lengo la kuboresha afya ya uzazi na ustawi wa jamii.









# MHAGAMA AKABIDHI VITENDEA KAZI VYA SH. MILIONI 674.3 KWA WAHUDUMU WA AFYA NGAZI YA JAMII

!

**Na Hassan Kimweri**
**KAGERA**

Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama amekabidhi vitendea kazi kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii vyenye thamani ya Shilingi Milioni 674.3 kwa mikoa Saba ambayo ni Njombe, Pwani, Kigoma, Ruvuma, Songwe, Lindi pamoja na Kagera.

Waziri Mhagama alikabidhi vitendea kazi hivyo Januari 3, 2025 akiwa mkoani Kagera, mkoa ambao umewakilisha mikoa mengine Sita(6) itakayotoa huduma za afya kwa wananchi ikiwemo elimu juu ya magonjwa yasiyoambukiza na magonjwa ya milipuko.

"Vitendea kazi vilivyokabidhiwa ni pamoja na viatu maalum vya kazi, miamvuli, mabegi pamoja na sare maalum zitakazowatambulisha kuwa wao ni wahudumu wa afya ngazi ya jamii watakaokuwa wawili katika kila kitongoji (mwanamke na mwanaume)," alisema Waziri Mhagama.

Waziri Mhagama alisema, mpango huo wa wahudumu wa afya ngazi ya jamii ni mpango wa Taifa unaoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, lengo likiwa ni kuhakikisha hadi ifikapo mwaka 2028 Tanzania inakuwa na wahudumu hao wapatao 137,294 nchi nzima ili kupunguza magonjwa.

Aidha, Waziri Mhagama alisema katika kipindi kifupi cha uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali imewezesha uwepo wa dawa pamoja na vifaa tiba ikiwemo vifaa vya uchunguzi ambavyo vinatumia tekinolojia ya hali ya juu.

"Sasa hivi kuna ongezeko la mashine ya uchunguzi wa magonjwa MRI 14, CT-Scan 45, Digital X- Ray 439, Ultrasound zaidi ya 600 pamoja na Pet-Sacan 1 mpya yenye thamani ya zaidi ya Shilingi Bilioni 18 ambayo tumeifunga pale kwenye Taasisi ya Saratani Ocean Road kwa ajili ya wagonjwa wa kansa," alisema Waziri Mhagama.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Kagera Mhe. Hajat Fatuma Mwasa aliishukuru Serikali ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Sekta ya Afya kwa uendelea kuboresha miundombinu pamoja na upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba ambavyo vinawahudumia wananchi wa mkoa huo katika masuala ya afya.



# WAZIRI MHAGAMA AGAWA MASHINE 185 ZA UCHUNGUZI WA KIFUA KIKUU NCHI NZIMA

**Na Cletus Sanga**
**DODOMA**

Katika jitihada za kudhibiti na kutokomeza ugonjwa wa Kifua Kikuu nchini Tanzania ifikapo 2030, Serikali imegawa mashine mpya 185 zenye thamani ya Shilingi Bilioni 7 kwa ajili ya uchunguzi na ugunduzi wa vimelea vya ugonjwa huo nchini.

Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama alisema hayo Januari 6, 2025 kwenye hafla ya ugawaji wa mashine hizo iliyofanyika katika Kituo cha Afya Chamwino, Dodoma iliyoenda sambamba na uzinduzi wa Mpango harakishi wa kuibua wagonjwa wa Kifua Kikuu katika Halmashauri 76 za mikoa tisa (9).

Waziri Mhagama alisema Tanzania inafanya vizuri kwenye mapambano dhidi ya ugonjwa wa Kifua Kikuu ambapo kwa sasa ni nchi ya Sita(6) kati ya nchi zote zinazofanya vizuri, lakini bado juhudi zinaendelea ili kufanya vizuri zaidi kwa kuwa bado tupo ndani ya nchi 30 zenye maambukizi makubwa.

"Ugonjwa wa Kifua Kikuu bado ni ugonjwa tishio nchini na ulimwenguni kwa ujumla kwa kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi 30 zenye maambukizi makubwa ya ugonjwa huo ambazo kwa pamoja zinachangia asilimia 87 ya wagonjwa wote wa Kifua Kikuu Duniani," alisema Waziri Mhagama.

"Leo tunazindua mashine za kisasa 75 aina ya GeneXpert zinazotumika katika ngazi ya Hospitali, na mashine 110 aina ya Truenat ambazo zimetengenezwa kuwezesha kufanya kazi hadi katika ngazi ya Zahanati ambazo zimegharimu Shilingi Bilioni 7 na zitasambazwa katika mikoa yote na mikoa miwili (2) upande wa Zanzibar," alifafanua Waziri Mhagama.

Katika hatua nyingine Waziri Jenista alizindua Mpango harakishi wa kuibua wagonjwa wa Kifua Kikuu kwenye Halmashauri 76 kutoka mikoa 9 ambayo kwa 2024 ilionyesha kuwa na kiwango kidogo cha uibuaji wa wagonjwa ikilinganishwa na miaka ya nyuma ambao ni mkoa wa Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Kagera, Mara, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu na Tanga.

Naye Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. Ahmad Makuwani alisema kuwa juhudi kubwa sasa zinaelekezwa katika uibuaji wa wagonjwa wapya wa Kifua Kikuu, Serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika teknolojia ya matibabu hasa kwenye vifaa tiba, hivyo sasa tuna jukumu la kutoacha mtu nyuma kwenye mapambano hayo na kutokomeza Kifua Kikuu ifikapo mwaka 2030.

Wizara ya Afya

# FAHAMU KUHUSU UGONJWA WA UKOMA



Ukoma ni Ugonjwa unaosababishwa na vimelea vinavyoshambulia mishipa ya fahamu na huambukizwa kwa njia ya hewa pekee na siyo kwa kugusana au kushikana mikono.

"Tokomeza Ukoma, Pinga Unyanyapaa na Imarisha ustawi wa Afya ya Akili"





Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
WIZARA YA AFYA, TANZANIA, TOLEO LA MWEZI JANUARI, 2025